JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAZIRI MKUU
## KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

www.kazi.go.tz

Toleo la 8 | Septemba, 2022



## MAONESHO ya NGUVU KAZI / JUA KALI

**Wajasiriamali 250 kuwezeshwa usafiri na Rais Samia kushiriki Maonesho ya Jua Kali Uganda.**

*Mhe. Samia Suluhu Hassan*

RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA




## RAIS SAMIA KUWEZESHA USAFIRI WA WAJASIRIAMALI WADOGO KUSHIRIKI MAONESHO YA JUA KALI UGANDA

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu- Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Mhe. Prof. Joyce Ndalichako amesema Mhe.Rais Samia Suluhu Hassan atawezesha usafiri wa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati 250 kushiriki Maonesho ya 22 ya Wajasiriamali Wadogo na wa Kati wa Jumuiya ya Afrika Mashariki maarufu kama Nguvu Kazi au Jua Kali yatakayofanyika Jijini Kampala, Uganda kuanzia tarehe 8 hadi 18 mwezi Desemba 2022.

“Kipindi cha miaka mingi, pamoja na mambo mengine, serikali imekua ikichangia usafiri wa mizigo ya Wajasiriamali kwenda kwenye maonesho. Kwa mwaka huu, Serikali yetu inayoongozwa na Mhe. Rais Samia imepanga kuongeza mchango wake kwa kuwezesha usafiri wa basi la wajasiriamali kwenda na kurudi Uganda,“

Mhe. Ndalichako amefafanua kuwa serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu itatumia maonesho hayo kwa lengo la kuwawezesha vijana wajasiriamali wa Tanzania kutumia fursa hiyo kutafuta masoko katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kuwawezesha vijana kujiajiri na hivyo kukuza ajira na kuondoa umaskini.

Akiongea na Waandishi wa habari jijijini Dodoma, tarehe 21 Septemba, 2022, Mhe. Waziri Ndalichako amesema Ofisi hiyo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwezeshaji - Zanzibar, Wizara, Taasisi nyingine za Serikali na Shirikisho la Vyama vya Wajasiriamali imejipanga kukahikisha inaibua vijana wajasiriamali mahiri wakiwemo watu wenye ulemavu watakaoiwakilisha Tanzania katika maonesho

*Inaendelea Uk. 2*



Kauli mbiu ya maonesho ya mwaka huu ni "Nunua Bidhaa au Huduma za Afrika Mashariki ili Kuijenga Afrika Mashariki kwa Ustahimilivu na Maendeleo Endelevu"

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama Vya Wajasiriamali Wadogo Tanzania ambaye pia ni Mwenyekiti wa Shirikisho Wajasiriamali Wadogo na wa Kati wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Joseph Rweyemamu, ameshukuru kwa jitihada ambazo serikali imeendelea kuzifanya katika kuhakikisha wanashiriki maonesho hayo. Aidha, ameahidi kutangaza bidhaa za Tanzania, Utalii pamoja na lugha ya kiswahili.

Wajasiriamali wapatao 1,000 kutoka Burundi, Kenya, Rwanda, Uganda, Sudan ya Kusini, Jamhuri ya Demokrasia ya Congo na Tanzania ikiwa mojawapo watashiriki maonesho hayo.Aidha, wito umetolewa kwa Wajasiriamali wa Tanzania kujitokeza kushiriki maonesho.

Fomu za maombi pamoja na maelekezo kwa Wajasiriamali wanaokusudia kushiriki maonesho haya zitapatikana kuanzia tarehe 26 Septemba, 2022 katika Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya na Manispaa kote nchini na pia katika tovuti ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu: www.kazi.go.tz.

Aidha, fomu hizo pia zitapatikana kupitia Shirikisho la Vyama vya Wajasiriamali Wadogo ila zote zitapaswa kurudishwa kupitia Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa. Mwisho wa kurudisha fomu kupitia Halmashauri husika ni tarehe 17 Oktoba, 2022.



# UJENZI MJI WA SERIKALI WAONGEZA FURSA ZA AJIRA

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa amesema ujenzi wa mradi wa Mji wa Serikali unaondelea jijini Dodoma umesaidia kuongeza fursa za ajira na maendeleo kwa wananchi kwa kuwawezesha kufanya shughuli zinazowaingizia kipato.

Mhe. Waziri Mkuu ameeleza hayo leo Septemba 5, 2022 mara baada ya kukamilisha ziara yake ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Mji wa Serikali, Mtumba jijini Dodoma.

Ameeleza kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan inafanya jitihada za ushirikishwaji wananchi katika miradi ili waweze kujikwamua kiuchumi.

"Tumeendelea kuona jitihada za Mhe. Rais Samia za kutekeleza miradi ya maendeleo. Jitihada hizo zinasaidia kutatua changamoto za ajira nchini.Katika mradi huu wapo vijana mafundi waliopata ajira lakini pia yapo makundi ya wanawake na wanaume wanaofanya biashara hali inayo wawezesha kujiongezea kipato"

Aidha, Mheshimiwa Waziri Mkuu amewataka vijana wanaofanya kazi katika mradi huo wa ujenzi wa Mji wa Serikali Mtumba, kuhakikisha ujuzi walioupata wanautumia katika kutekeleza miradi mingine kama hiyo, kwa kuwa hadi kukamilika kwa mradi huo watakuwa na wanaoujuzi wa kutosha.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Mhe. Prof. Joyce Ndalichako amesema kuwa mradi huo wa ujenzi wa Mji wa Serikali umekuwa ukizalisha ajira za moja kwa moja na mabazo sio za moja kwa moja.

"Katika Ujenzi wa Majengo yote ya Serikali unaoendelea hapa Mtumba, ajira 120 zinazalishwa kwa siku, ambapo wananchi wanaoshiriki katika ujenzi huu wanaweza kujikwamua kiuchumi kupitia ajira hizo"





# WADAU WAHAMASISHWA KUCHANGIA TIMU YA TEMBO WARRIORS

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Patrobas Katambi amewahamisisha wadau kujitokeza na kuchangia timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Watu wenye Ulemavu - Tembo Warriors ili ifanikiwe kushinda mashindano Kombe la Dunia nchini Uturuki ambayo itashiriki michuano hiyo mwaka huu itakayoanza Septemba 30 hadi Oktoba, 09 nchini humo.

Mhe. Katambi akiongea na Timu hiyo kwa lengo la kuwahamasisha na kuwaaga kuelekea nchini Uturuki kwa maandalizi ya michuano hiyo, amefafanua kuwa Serikali inayoongozwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan ipo pamoja na Watu wenye Ulemavu na imetoa zaidi ya Mil. 150, ili kuhakikisha wanapata ushindi katika michuano hiyo.

“Tunaomba wadau hususani Taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali, Sekta Binafsi tuwasaidie timu ya Tembo warriors ili wawe washindani kwenye michuano hiyo

Ameongeza kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu itaendelea kuwahamasisha wadau kuisaidia timu hiyo ili iweze kuimarika kimataifa na kuiweka nchi ya Tanzania katika Ramani ya michezo kimataifa.





## WADAU WAPITIA NYARAKA ZA STADI ZA MAISHA KWA VIJANA NJE YA SHULE

Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu Prof. Jamal Katundu amefungua kikao kazi cha wadau kwa lengo la kupitia, kutoa maoni na kuthibitisha rasimu ya Mwongozo, viwango sanifu na mfumo wa utekelezaji wa Programu ya Stadi za Maisha kwa vijana nje ya shule.

Profesa Jamal amesema hayo jijini Dodoma alipokuwa akifungua kikao kazi hicho na kueleza kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu ilianza kufanya mapitio ya Mwongozo wa Stadi za Maisha wa mwaka 2009 kwa lengo la kuhakikisha masuala mapya yanayojitokeza katika duru za kimataifa, kikanda na kitaifa kwa ajili ya maendeleo ya vijana yanahuishwa kwenye mwongozo huo.

“Stadi za Maisha ni elimu, mbinu na maarifa ambayo hutolewa kwa vijana kwa lengo la kuhamasisha mabadiliko chanya ya tabia, hivyo utekelezaji wa mwongozo huu utasaidia kutengeneza afua madhubuti zitakazo wawezesha vijana kushughulikia changamoto nyingi zinazowakumba," amesema

Amefafanua kuwa, Serikali kupitia wizara yenye dhamana na maendeleo ya vijana iliona umuhimu wa kuwa na mwongozo huo kwa kuweka mfumo wa uratibu, ufuatiliaji, tathmini na taarifa za utekelezaji ili kusaidia kwa kiasi kikubwa kufanikisha utekelezaji wa programu hiyo ya stadi za Maisha kwa vijana nje ya shule.

Sambamba na hayo, Prof. Jamal Katundu ameshukuru Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) kwa ushirikiano na Serikali katika kufanikisha utekelezaji wa programu za maisha kwa vijana hapa nchini.

Kikao kazi hicho kitafanyika kwa siku mbili kuanzia tarehe 29 hadi 30 Septemba, 2022 ambapo wadau hao watapitia nyaraka mbalimbali ikihusisha Mwongozo na Viwango sanifu vya utoaji wa elimu ya stadi za maisha pamoja na mfumo wa uratibu, ufuatiliaji, tathmini na taarifa za utekelezaji wa programu hiyo.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Prof. Joyce Ndalichako akiteta jambo na Naibu Katibu Mkuu wa TUICO, Bw. Tamim Salehe mara baada ya kufungua semina kwa Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA) kuhusu uelewa wa kanuni mpya ya mafao ya pensheni, jijini Dodoma.*

*Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Patrobas Katambi akizungumza na wachezaji wa Timu ya Tembo Warriors alipokutana nao kwa lengo la kuwahamasisha kuelekea kwenye michuano ya kombe la dunia kwa Watu wenye Ulemavu nchini Uturuki.*





*Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Prof. Jamal Katundu kwenye picha ya pamoja na wadau mara baada ya kufungua kikao kazi cha kupitia na kutoa maoni kuhusu rasimu ya Mwongozo, Viwango Sanifu na Mfumo wa utekelezaji wa Programu ya Stadi za Maisha kwa vijana nje ya shule.*

KATIBU MKUU
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU**
S.L.P 2890
**DODOMA, Tanzania**
Barua pepe: ps@kazi.go.tz
**www.kazi.go.tz**
@Ofisi ya Waziri Mkuu_Kazi

**Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**